## UVM Usimamizi wa Matibabu ya Wagonjwa
## Haki na Majukumu Yako

**Haki Zako**

- Kupata habari kuhusu afya inayoeleweka kirahisi
- Kutendewa kwa fadhili na heshima
- Kushirikiana kufanya maamuzi kuhusu matibabu
- Kujua kwamba habari zako za kibinafsi zinatunzwa kama siri, na jinsi tunavyofanya hivyo
- Kuuliza maswali kuhusu programu yetu
- Kujifunza kuhusu huduma zinazopatikana, na mambo unayoweza kuchagua
- Kujua kuna nani kwenye timu yako ya matibabu
- Kupata mkalimani bila malipo ukihitaji
- Kushiriki maelezo au malalamiko kuhusiana na usalama*
- Kutoka kwa programu hiyo ya kupokea huduma wakati wowote

**Majukumu Yako**

- Kumpatia msimamizi wa matibabu yako habari zitakazomsaidia
- Kuuliza maswali ikiwa kuna jambo ambalo huelewi
- Kuwaambia watu wa timu yako ya matibabu ikiwa mpango wako wa matibabu ni vigumu kufuata
- Kutujulisha ikiwa ungependa kuacha kupokea huduma hizo

## UVM Kikundi cha Kushirikiana ili Kupata Matibabu
## Heshima na Kuwahusisha Wote

**Tafadhali uwe mwenye heshima**

- Uwe mwenye fadhili kwa wafanyakazi, wagonjwa, na watu wanaotembelea
- Uonyeshe ufikirio kupitia maneno na matendo
- Tuko hapa ili kukusaidia katika nyakati ngumu

**Haturuhusu**

- Kutenda kwa njia inayokosa adabu au kwa njia ya kutisha
- Kusema mambo mabaya kumhusu mtu yeyote kwa sababu ya: jamii, jinsia, dini, utamduni, ulemavu, umri, hali ya kuwa na ukimwi, kutumika kwa jeshi, au hali yake ya uhamiaji

**Kuomba mfanyakazi mwingine**

- Haturuhusu watu kuomba mfanyakazi mwingine kwa sababu zinazotegemea ubaguzi
- Katika visa vya pekee (kama vile ikiwa umepitia mambo mabaya wakati uliopita au sababu za kidini), huenda tutafikiria kwa makini ikiwa utaweza kupewa mfanyakazi mwingine

- Watu wanaopokea huduma zetu wanaruhusiwa kukataa kutibiwa na wafanyakazi wanaowafahamu kibinafsi au wanaowafahamu kwa njia isiyo rasmi.

  * Ikiwa una mambo yoyote ambayo ungependa kutuelezea, maelezo, au malalamiko, unaweza kutupigia bila malipo kwa (833)763-0652